

**HOTUBA YA MHE. CHARLES MAKONGORO NYERERE  
MKUU WA MKOA WA RUKWA WAKATI WA UFUNGUZI WA  
KIKAO CHA KWANZA CHA KAMATI YA USHAURI YA MKOA  
(RCC) KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KATIKA UKUMBI  
WA RDC TAREHE 06 OKTOBA, 2023**

- *Mwenyekiti wa CCM Mkoa,*
- *Katibu Tawala Mkoa,*
- *Katibu wa CCM Mkoa,*
- *Wahe. Wabunge,*
- *Kamati ya Usalama Mkoa,*
- *Wakuu wa Seksheni na Vitengo wa Sekretarieti ya Mkoa,*
- *Wakuu wa Taasisi za Serikali,*
- *Mstahiki Meya wa Manispaa ya Sumbawanga,*
- *Wahe. Wenyeviti wa Halmashauri (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),*
- *Makatibu Tawala wa Wilaya (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi)*
- *Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga,*
- *Wakurugenzi wa Halmashauri (Sumbawanga, Kalambo na Nkasi),*
- *Wakuu wa Taasisi binafsi,*
- *Viongozi wa Dini,*
- *Wazee Maarufu,*

- ***Viongozi wa vyama vya siasa,***
- ***Wageni waalikwa,***
- ***Waandishi wa Habari,***
- ***Mabibi na Mabwana.***

## **Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

Awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana leo katika kikao hiki muhimu kwa ajili ya Maendeleo ya Mkoa wetu wa Rukwa. Natambua kuwa miongoni mwa Wajumbe na wageni waalikwa wametoka mbali na Sumbawanga, kwa kutambua hilo naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwasafirisha salama na niwakaribishe sana Sumbawanga.

***Ndugu Wajumbe,*** Kikao hiki ni cha kwanza tangu Mhe. Rais Dkt Samia Suluhu Hassan aniamishie katika Mkoa huu wa Rukwa. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa Imani yake kubwa kwangu na mimi namuahidi kuwa sitamuangusha katika utekelezaji wa majukumu yangu. Rai yangu kwa Watendaji wa Serikali ni kuhakikisha kuwa mnashirikiana katika utekelezaji wa Majukumu yenu ili kutimiza lengo la Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan la kuwaletea Wananchi Maendeleo.

***Ndugu Wajumbe,*** Mkoa wa Rukwa tunaendelea kumshukuru sana na kumuunga mkono Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutupatia fedha nyingi kwa ajili ya miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika kipindi cha Januari – Desemba, 2022 na Januari – Juni, 2023 tumepokea fedha nyingi sana kwenye miradi ya maendeleo (Miradi ya Elimu Bilioni 21.9, Utawala Bora Bilioni 3, Miradi ya Afya Bilioni 6.7, Miradi ya Barabara za TARURA Bilioni 10.7, Miradi ya Maji Bilioni 32.1, Miradi ya Barabara za TANROADS Bilioni 10.8 pamoja na kuanza ujenzi wa Uwanja wa Ndege Sumbawanga kwa gharama ya Shilingi Bilioni 55. Aidha, TANROADS wameanza ujenzi wa barabara ya Ntendo – Kizungu na Matai – Tatanda kwa gharama ya Shilingi Bilioni 82.6

Nitoe maelekezo kwa Wakurugenzi na Wakuu wa Wilaya kuhakikisha kuwa miradi yote ya Elimu inakamilika ifikapo tarehe 30 Oktoba, 2023. Aidha, Halmashauri ziweke Mpango Kazi wa kukamilisha miradi yote viporo.

***Ndugu Wajumbe,*** Katika kipindi cha mwezi Mei, 2023 Wanafunzi **1,978** wa Kidato cha Sita walifanya Mtihani wa Taifa Kati ya Wanafunzi hao waliofanya Mtihani waliopata Daraja la Kwanza ni Wanafunzi **543** Daraja la **Pili 1,131** Daraja la Tatu **302** Daraja la Nne **2** na Daraja Sifuri **0**. Tunawapongeza sana Walimu wetu wote ambao walijituma sana na kuhakikisha kuwa Wanafunzi wetu wanafaulu vizuri.

***Ndugu Wajumbe***, Mwezi Agosti, 2022 ilifanyika Sensa ya Watu na Makazi Tanzania. Mkoa wetu wananchi walishiriki kuhesabiwa na kuhamasisha wenzao kuhesabiwa. Baada ya matokeo ya Sensa Mkoa wetu ulibainika kuwa na Watu 1,539,519 ambapo kwa Majimbo ni kama ifuatavyo: **Nkasi Kaskazini 247,286, Nkasi Kusini 178,134, Sumbawanga Mjini 303,986, Kalambo 316,783 na Kwela 494,330**. Nitumie fursa hii kuwashukuru Viongozi wote kwa namna mlivyojitoa kuhamasisha Wananchi wengi kujitokeza. Pili niwashukuru Wananchi wote kwa kujitokeza kuhesabiwa.

***Ndugu Wajumbe***, Katika kuhakikisha TRA na Halmashauri zetu zinakusanya Mapato ya kutosha. Katika Kipindi cha Januari – Desemba, 2022 na Januari – Juni, 2023 TRA ilikusanya shilingi Bilioni 37.8 sawa na asilimia 106 ya lengo la kukusanya shilingi Bilioni 35.6. Kwa upande wa Mamlaka za serikali za Mitaa kwa kipindi cha mwezi Januari –Desemba, 2022 na Januari – Juni, 2023 Halmashauri zetu zilikusanya shilingi Bilioni 14.6 sawa na asilimia 95.4 ya kukusanya shilingi Bilioni 15.3. Niwaombe wanarukwa wote tuendeleo kulipa kodi kwani faida ya kulipa kodi tunaiona kwa kuletewa fedha za Miradi ya Maendeleo. Niwaombe tu kuwa **“Ukiuza toa risiti na ukinunua dai risiti”**

Nimalizie kwa kuwashukuru wote kwa kunisikiliza. Aidha, ni Imani yangu kuwa katika kikao hiki kila mjumbe atachangia

mawazo yake kwa maendeleo ya Mkoa wetu. Baada ya kusema hayo nitamke sasa kuwa Kikao cha Kwanza cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kwa Mwaka 2023/2024 nimekifungua rasmi.

Mungu ibariki Tanzania,  
Mungu Bariki Mkoa wetu wa Rukwa.

Asanteni kwa kunisikiliza.

Charles Makongoro Nyerere  
**MKUU WA MKOA WA RUKWA**